

**SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU
TANZANIA.**

KATIBA

**TANZANIA BASKETBALL FEDERATION
TBF**

21ST OCTOBER, 2001

SURA YA KWANZA: JINA, MAKAO MAKUU, MATUMIZI, TAFSIRI NA MADHUMUNI

Ibara ya	1	Jina	Ukurasa	2
Ibara ya	2	Makao Makuu	Ukurasa	2
Ibara ya	3	Matumizi ya Katiba	Ukurasa	2
Ibara ya	4	Tafsiri	Ukurasa	2
Ibara ya	5	Madhumuni na Mhimili	Ukurasa	2

SURA YA PILI: UANACHAMA

Ibara ya	6	Aina ya Uanachama	Ukurasa	3
Ibara ya	7	Kujiunga, Uanachama, Viingilio	Ukurasa	4
Ibara ya	9	Kupoteza Uanachama	Ukurasa	4
Ibara ya	10	Kurudishiwa Uanachama	Ukurasa	4

SURA YA TATU: MUUNDO WA SHIRIKISHO

Ibara ya	11	Mikoa	Ukurasa	3
Ibara ya	11	Vyombo vya Shirikisho	Ukurasa	4
Ibara ya	12	Mkutano Mkuu	Ukurasa	5
Ibara ya	13	Wajumbe wa mkutano mkuu	Ukurasa	5
Ibara ya	14	Kazi za mkutano mkuu	Ukurasa	5
Ibara ya	15	Bodi ya shirikisho	Ukurasa	5
Ibara ya	16	Wajumbe wa Bodi ya shirikisho	Ukurasa	5
Ibara ya	17	Kazi na wajibu wa Shirikisho	Ukurasa	6
Ibara ya	18	Kamati ya Utendaji	Ukurasa	6
Ibara ya	19	Wajumbe wa kamati ya Utendaji	Ukurasa	6
Ibara ya	20	Kazi na wajibu wa kamati ya Utendaji	Ukurasa	6
Ibara ya	21	Kamisheni za Shirikisho	Ukurasa	7
Ibara ya	22	Wajumbe wa Kamisheni	Ukurasa	7
Ibara ya	23	Kazi za kamisheni ya Makocha	Ukurasa	7
Ibara ya	24	Kazi za Kamisheni ya waamuzi	Ukurasa	7
Ibara ya	25	Kazi za Kamisheni ya watoto wadogo na Maendeleo ya Mashule	Ukurasa	8
Ibara ya	26	Kazi za Kamisheni ya Wanawake	Ukurasa	8
Ibara ya	27	Kazi za Kamisheni ya Mipango na Maendeleo	Ukurasa	8
Ibara ya	28	Kazi za Kamisheni ya Walemavu	Ukurasa	8
Ibara ya	29	Kazi za Kamisheni ya tiba ya Wanamichezo	Ukurasa	9
Ibara ya	30	Kazi za Kamisheni ya ufundi na Uendeshaji wa Mashindano	Ukurasa	9

SURA YA NNE:

UCHAGUZI

Ibara ya	31	Mkutano Mkuu wa Uchaguzi	Ukurasa	10
Ibara ya	32	Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi	Ukurasa	10
Ibara ya	33	Sifa za Wagombea	Ukurasa	10
Ibara ya	34	Kipindi cha Uongozi	Ukurasa	11

SURA YA TANO

VIONGOZI WA SHIRIKISHO, KAZI NA MADARAKA

Ibara ya	35	Viongozi wa Shirikisho	Ukurasa	11
Ibara ya	36	Kazi, Madaraka na Wajibu wa Viongozi	Ukurasa	11
Ibara ya	37	Mlezi na Baraza la Wadhamini	Ukurasa	13

**SURA YA SITA
MIGOGORO NA RUFAA**

Ibara ya 38 Migogoro Ukurasa 13

SURA YA SABA: FEDHA ZA SHIRIKISHO

Ibara ya 39 Mapato Ukurasa 13
Ibara ya 40 Matumizi Ukurasa 14
Ibara ya 41 Hesabu Ukurasa 14

**IBARA YA NANE
HATI MILIKI, LUGHA, NEMBO NA BENDERA**

Ibara ya 42 Bendera Ukurasa 14
Ibara ya 43 Nembo Ukurasa 14
Ibara ya 44 Lugha rasmi Ukurasa 15
Ibara ya 45 Uamuzi kuvunja shirikisho Ukurasa 15
Ibara ya 46 Kupitisha Katiba Ukurasa 15

SURA YA 1

JINA, MAKAO MAKUU, MATUMIZI, TAFSIRI NA MADHUMUNI

IBARA YA 1

JINA

Jina la Chama litakuwa: SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA- (TANZANIA BASKETBALL FEDERATION) kwa kifupi TBF. Jina hili ni badala ya Basketball Association of Tanzania kwa kifupi BATA

IBARA YA 2:

Makao makuu ya Shirikisho yatakuwa katika mji wa Dar es Salaam. S.L. P 20116, DAR ES SALAAM

MAKAO

IBARA YA 3

MATUMIZI:

Katiba hii itatumiwa na Wanachama na kuendesha shughuli zote zinazosimamamia mpira wa kikapu nchini Tanzania. Wanachama watakuwa na katiba zao ambazo hazitakuwa zinapingana na katiba hii.

IBARA YA 4

TAFSIRI:

Maana ya maneno katika katiba hii, isipokuwa pale ambapo imeainishwa vinginevyo

TBF:

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania au Tanzania Basketball Federation

SHIRIKISHO

BMT

Maana yake ni Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania Baraza la Michezo Taifa

MSAJILI:

Msajili wa vilabu na vyama vya michezo

MIKOA

Kiutawala ni wanachama na msingi katika shirikisho.

FIBA:

Shirikisho la Mchezo wa Kikapu Ulimwenguni (Federation Internationale de Basketball)

WAZIRI:

Maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia michezo

BODI:

Chombo cha Utawala katika Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania

KAMATI:

Sekretariati ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania

KAMISHENI:

Kamati zinazoshikilia maeneo ya ufanisi katika Shirikisho.

KLABU:	Ni kundi la msingi la awali lililo jikusanya na kujisajili kwa madhumuni ya kucheza mpira wa Kikapu
TOC:	Kamati ya Olimpiki ya Tanzania, au Tanzania Olympic Committee.
ECSABC:	Shirikisho la Mpira wa Kikapu wa Nchi za Mashariki, kati na kusini mwa Afrika, au East Central and Southern African Basketball Confederation.
AFABA:	Shirikisho la Mpira wa Kikapu la Afrika au

IBARA YA 5 MADHUMUNI

- TBF itajishughulisha na kujihusisha na Uhamasishaji, ukuzaji, na udhibiti wa masuala yote yanayohusu mchezo wa mpira wa Kikapu Tanzania. Bila kupotosha msingi huo, TBF itakuwa na madhumuni yafuatayo:
- 5.1 Kuongoza na kusimamia shughuli zote za mpira wa kikapu.
 - 5.2 Kudhibiti na kusimamia uteuzi wa walimu, waamuzi na wakufunzi wa mpira wa kikapu.
 - 5.3 Kukuza na kuendeleza maeneo yote ya ufanisi kwa kushirikiana na mikoa yote.
 - 5.4 Kushirikiana na mikoa kuhakikisha vyama hivyo vinadhibiti shughuli zote za mpira wa kikapu zinazo fanyika katika maeneo yao.
 - 5.5 Kudhibiti usajili na kuhama kwa wachezaji.
 - 5.6 Kuandaa na kusimamia ushiriki wa timu za Tanzania kwenye michezo ya kimataifa.
 - 5.7 Kuunda na kuandaa timu za taifa za mpira wa kikapu.
 - 5.8 Kubuni, kukuza, kuendeleza na kutekeleza programu za kiufundi na maendeleo yao.
 - 5.9 Kusimamia ustawi wa vilabu, wilaya, mikoa na vyama vishiriki katika maendeleo yao.
 - 5.10 Kuwa na mpango wa kupata viwanja na vifaa vya mchezo huu vyenye viwango vya kimataifa.
 - 5.11 Kufanya jambo lolote muhimu kwa manufaa ya maendeleo ya mpira wa kikapu.

MUHIMILI WA SHIRIKISHO

TBF litakuwa ndiyo Shirikisho pekee lililo ruhusywa kisheria kuongoza na kusimamia shughuli zote za Mpira wa Kikapu kwa Wanaume na Wanawake katika Tanzania. Shirikisho litaundwa na Mikoa na Vyama vishiriki ambavyo vina mamlaka kisheria ya kusimamia mchezo wa Mpira wa Kikapu katika Maeneo yanayohusika. TBF inatambuliwa na BMT na imeshirikishwa katika TOC, ESCABC, AFABA na FIBA. TBF haitajihusisha na ubaguzi wa aina yoyote kati ya wachezaji, viongozi, wanachama na wala haitajihusisha na masuala ya Kidini au ya kisiasa.

SURA YA II UANACHAMA

IBARA YA 6

AINA YA WANACHAMA

- 6.1 Uanachama wa msingi
- 6.2 Uanachama wa Kujishirikisha
- 6.3 Uanachama wa heshima

- 6.4 WANACHAMA
- 6.4.1 Shirikisho litaundwa na mikoa ambayo ndio wanachama wake wa msingi. Hawa ndio wanaofanya shirikisho lifanye kazi zake za kila siku.
- 6.4.2 Mikoa itasajiliwa chini ya sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya 1971 ya BMT, pamoja na kanuni zake Na. 442 za mwaka 1999.
- 6.4.3 Mikoa inaundwa na Vilabu vinavyojihusisha na mpira wa kikapu na vilivyo sajiliwa na Msajili.
- 6.4.4 Mikoa ya Shirikisho ina hadhi sawa, kila mkoa una mamlaka kamili katika eneo lake.
- 6.4.5 Mikoa itaheshimu katiba ya shirikisho na kutekeleza kanuni, sheria na maamuzi yote ya TBF.
- 6.4.6 Mikoa itakuwa na dhamana ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya shirikisho.
- 6.4.7 Mikoa itatekeleza wajibu wake kwa kuendeleza mpira wa kikapu katika mikoa na kushirikiana na vyombo vingine vya shirikisho, ili kuboresha ukuaji na ustawi wa mchezo huu.

- 6.5 UANACHAMA WA KUJISHIRIKISHA
Kutakuwa na wanachama wa kujishirikisha. Vyama vya kitaalamu vya Mpira wa kikapu vitakuwa ni wanachama wa kujishirikisha ikiwa ni pamoja na:
 - 6.5.1 Chama cha waalimu wa Mpira wa Kikapu Tanzania
 - 6.5.2 Chama cha waamuzi wa mpira wa Kikapu Tanzania
 - 6.5.3 Asasi za michezo ngazi ya taifa zinazojihusisha na mpira wa kikapu kama ilivyo ainishwa katika katiba ya asasi hizo.
- 6.6 WANACHAMA WA HESHIMA
- 6.6.1 Kutakuwa na wanachama wa heshima wa TBF. Bodi ya Shirikisho inaweza kutoa uanachama wa heshima kwa watu mashuhuri waliotoa mchango uliotukuka kwa shirikisho, au Chama cha hiari au Taasisi yoyote kutokana na mchango wao kwenye maendeleo ya mpira wa kikapu.

IBARA YA 7

KUJIUNGA UANACHAMA, ADA NA VIINGILIO.

- 7.1 Kila anayetaka kuwa mwanachama atatuma maombi yakiambatana na kiingilio na ada ya Uanachama kabla ya kukubaliwa.
- 7.2 Kutakuwa na kiingilio kwa mwanachama mpya na ada ya kila mwaka.
- 7.3 Viwango vya ada na viingilio vitapangwa na Bodi na vinaweza kubadilishwa inapobidi kufuatia mabadiliko ya kanuni za Shirikisho.
- 7.4 Maombi ya uanachama yakikataliwa kwa sababu zozote; Katibu Mkuu atamjulisaha aliyekataliwa maombi yake akimtaka kasoro zilizopo. Ada zitarudishwa iwapo maombi yatakataliwa kabisa.
- 7.5 Kila mwanachama wa kujishirikisha, atatuma maombi kwa katibu mkuu wa TBF kwa kutumia fomu maalum.
- 7.6 Mwanachama mpya wa msingi atakubaliwa na kamati ya utendaji mara moja.

IBARA YA 8

HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

Mwanachama atakuwa na wajibu na haki zifuatazo:

- 8.1 Mwanachama atakuwa na haki ya kushiriki mikutanao ya shirikisho inayomhusu.
- 8.2 Kushiriki mashindano yanayoandaliwa na shirikisho yanayomhusu.
- 8.3 Atakuwa na haki ya kuchagua viongozi wa shirikisho katika ngazi yake.
- 8.4 Mwanachama atakuwa na haki ya kuomba uongozi na kuchaguliwa kwa mujibu wa katiba hii.

IBARA YA 9

KUPOTEZA UANACHAMA

Mwanachama kama alivyotajwa katika katiba hii, atapoteza haki na uanachama iwapo yatatokea mojawapo ya mambo yafuatayo:-

- 9.1 Atashindwa kulipia ada ya uanachama katika muda uliopangwa.
- 9.2 Atafutwa na kusimamishwa na msajili kwa mujibu wa sheria ya BMT.
- 9.3 Atakiuka na kuvunja masharti ya TBF.
- 9.4 Atakiuka na kuvunja kwa makusudi katiba ya TBF kiasi cha kuathiri maendeleo ya mpira wa kikapu nchini.

IBARA YA 10

KURUDISHIWA UANACHAMA

- 10.0 Mwanachama aliyepoteza uanachama wa TBF kama ilivyo katika ibara ya 9 anaweza kurejeshewa uanachama wake iwapo:
 - 10.1 Atalipa ada zote alizokuwa akidaiwa
 - 10.2 Atarejeshewa au kusajiliwa upya na msajili.
 - 10.3 Atakiri na kuomba msamaha kwa maandishi kwenye bodi ya shirikisho kutokana na makosa yaliyofanya apoteze uanachama wake.

IBARA YA 11

VYOMBO VYA SHIRIKISHO:

Kutakuwepo na vyombo vifuatavyo katika shirikisho

- 11.1 Mkutano mkuu
- 11.2 Bodi ya Shirikisho
- 11.3 Kamati ya utendaji
- 11.4 Kamisheni za shirikisho
- 11.5 Mkutano mkuu wa uchaguzi

IBARA YA 12

MKUTANO MKUU

- 12 Kutakuwepo na mkutano mkuu wa shirikisho
- 12.1 Mkutano mkuu utaitishwa mara moja kila baada ya miaka 2 lakini unaweza kuitishwa kwa dharura endapo kuna haja na ulazima wa kufanya hivyo
- 12.2 Mkutano mkuu utaitishwa na Raisi wa Shirikisho baada

- ya Mashauriano na Katibu Mkuu.
- 12.3 Bodi ya shirikisho inaweza kwa maombi ya maandishi ya wajumbe wasiopungua nusu ya wajumbe wa Mkutano mkuu kuitisha kikao ikiona kuna haja na ulazima wa kufanya hivyo. Raisi wa TBF atalazimika kuitisha Mkutano Mkuu.
 - 12.4 Taarifa ya Mkutano mkuu sharti itolewe kwa maandishi kwa wajumbe sio chini ya mwezi mmoja kabla ya tarehe ya kikao.
 - 12.5 Idadi ya wajumbe kwenye mkutano Mkuu sharti isipungue zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa mkutano Mkuu wenye haki ya kupiga kura.
 - 12.6 Endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria haifikii kiwango zaidi ya nusu, mkutano utahairishwa kwa muda usiopungua siku 60.

IBARA YA 13

WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

Kutakuwepo na wajumbe wa mkutano mkuu wafuatao:

- 13.1 Raisi wa Shirikisho
- 13.2 Makamu wa Raisi wa Shirikisho
- 13.3 Wajumbe wote wa kamati ya utendaji
- 13.4 Mwenyekiti na katibu kutoka kila mkoa.
- 13.5 Mwenyekiti na katibu kutoka vyama vishiriki
- 13.6 Mchezaji mwakilishi kutoka kila mkoa

IBARA YA 14

KAZI ZA MKUTANO MKUU

Mkutano mkuu ndicho chombo chenye mamlaka ya juu kuliko vyombo vingine and ndicho kitakuwa na maamuzi ya mwisho katika mambo yote yanayohusu ustawi na maendeleo ya mpira wa kikapu.

- 14.1 Mkutano mkuu utabadilisha na kuthibitisha mabadiliko ya katiba
- 14.2 Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa zote za Bodi ya shirikisho zinazohusu uendeshaji wa shughuli za mpira wa kikapu.
- 14.3 Kusimamia, kuelekeza au kuagiza cha kufanya au kutekelezwa na vyombo vilivyo chini kwa maendeleo ya mpira wa kikapu.
- 14.4 Kurekebisha, kubadilisha, kuthibitisha na kuidhinisha uamuzi wowote uliotolewa na vyombo vya chini kama hapana budi.
- 14.5 Kuthibitisha nafasi yoyote ya uongozi itakayokuwa wazi kutokana na sababu mbalimbali.
- 14.6 Kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumvua madaraka kiongozi yeyote wa Taifa au ngazi ya chini, au kufuta uanachama wa mwanachama yeyote.

IBARA YA 15

BODI YA SHIRIKISHO

Bodi ya shirikisho ndiyo chombo cha juu cha Utawala wa Shirikisho kitakacho wajibika kwenye mkutano mkuu.

- 15.1 Bodi ya shirikisho itaitishwa mara mbili kila mwaka

- 15.2 Kunaweza kuitishwa kikao cha dharura endapo kutakuwa na haja na ulazima wa kufanya hivyo
- 15.3 Kikao cha Bodi kitaitishwa na Raisi wa Shirikisho baada ya kushauriana na kamati ya Utendaji.
- 15.4 Wajumbe wasiopungua nusu ya wajumbe wenye haki ya kupiga kura wanaweza kuomba kimaandishi kuitishwa kwa kikao.
- 15.5 Taarifa ya kikao cha Bodi sharti itolewe kwa maandishi sio chini ya siku 30 kabla ya tarehe ya kikao.
- 15.6 Endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria haifikii nusu ya kiwango cha wajumbe wote mkutano utahairishwa kwa muda usiopungua siku 30.

IBARA YA 16

WAJUMBE WA BODI YA SHIRIKISHO

- Kutakuwepo na wajumbe katika Bodi
- 16.1 Raisi wa shirikisho
- 16.2 Makamu wa Rais
- 16.3 Wajumbe wa kamati ya utendaji
- 16.4 Wenyeviti wa vyama vya mikoa wanachama wenyewe bila ya kuwakilishwa.

IBARA YA 17

KAZI NA WAJIBU WA BODI YA SHIRIKISHO

- Bodi ya TBF itakuwa na kazi na wajibu ufuatao
- 17.1 Bodi kitakuwa ndicho chombo chenye mamlaka ya juu kwa niaba ya mkutano mkuu, ambacho kitatekeleza kusimamia na kupanga utekelezaji wa shughuli za mpira wa kikapu nchini Tanzania
- 17.2 Kufanya matayarisho ya mkutano mkuu
- 17.3 Kupokea na kujadili taarifa za kamati ya utendaji na kuchukua hatua zipasazo.
- 17.4 Kupokea na kujadili taarifa za mikoa
- 17.5 Kutayarisha kutoa taarifa ya shirikisho
- 17.6 Kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya shirikisho mbele ya mkutano mkuu.
- 17.7 Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya mkutano mkuu.
- 17.8 Kujadili na kupitisha bajeti ya shirikisho.
- 17.9 Kupokea, kupanga na kuthibitisha kanuni za shirikisho
- 17.10 Kupokea na kuthibitisha sheria za michezo.
- 17.11 Kupendekeza majina matatu ya watu mashuhuri kwenye mkutano mkuu, watacao unda Baraza la wadhamini.
- 17.12 Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya kiongozi au uongozi wa chama au klabu, mwamuzi, na mchezaji kutokana na kukiuka kanuni za shirikisho au kanuni za uendeshaji Ligi au mashindano yeyote ya mpira wa kikapu.
- 17.13 Kujaza nafasi za uongozi zitakazo kuwa wazi, isipokuwa ile ya Raisi wa Shirikisho na makamu wake. Majina yaliyoteuliwa yatawasilishwa kwenye mkutano mkuu utakaofuata kwa kuthibitishwa.
- 17.14 Kusitisha uanachama wa mwanachama yeyote atakaye kiuka Katiba hadi suala hilo litakapo amuliwa vinginevyo na mkutano mkuu.
- 17.15 Kufanya kazi yoyote ile kwa manufaa na ustawi wa

- mpira wa kikapu nchini.
- 17.16 Kupendekeza hatua mwanafaka za kinidhamu dhidi ya mwanachama yeyote.

IBARA YA 18

KAMATI YA UTENDAJI

Kamati ya utendaji kitakuwa ni chombo cha watendaji wakuu wa kazi za kila siku za shirikisho. Kamati ya utendaji kwa maana ya ufanisi wa shirikisho, itakuwa ndiyo Sekretarieti ya TBF.

- 18.1 Kamati ya utendaji itakutana mara moja kila baada ya miezi miwili.
- 18.2 Kikao cha dharura cha kamati kinaweza kuitishwa endapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.
- 18.3 Kikao cha kamati ya utendaji kitaitishwa na katibu mkuu.
- 18.4 Iwapo katibu mkuu hataki au haelekei kuitisha kikao, basi wajumbe waliozidi nusu ya wajumbe wote wanaweza kutoa taarifa kwa raisi wa shirikisho atakaeitisha kikao hicho.
- 18.5 Taarifa ya maandishi ya kikao cha kamati, sharti itolewe siku 7 kabla ya kikao cha kamati.
- 18.6 Kiwango cha wajumbe kwenye kikao cha kamati, kitakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote.
- 18.7 Rais na makamo wa Raisi wa Shirikisho wanaweza kuhudhuria vikao vya sekretarieti.
- 18.8 Endapo akidi haitimii, au Mwenyekiti na Katibu hawatafika kwa sababu yoyote ile baada ya kuitisha kikao, kikao kitaahirishwa kwa muda usiopungua siku saba.

IBARA YA 19

WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI

Kutakuwepo na wajumbe wa kamati ya utendaji wafuatao:

- 19.1 Katibu Mkuu
- 19.2 Katibu Mkuu msaidizi
- 19.3 Mtunza Hazina
- 19.4 Makamishina Nane wa Shirikisho

IBARA YA 20

KAZI NA WAJIBU WA KAMATI YA UTENDAJI

Kamati ya Utendaji au sekretarieti itafanya kazi za kila siku za shirikisho

- 20.1 Kubuni na kupanga mbinu na utekelezaji wa maagizo ya Bodi ya shirikisho kwa ufanisi.
- 20.2 Kuhakiki kanuni za uendeshaji wa mashindano mbalimbali ya taifa na kuzipeleka kwenye bodi kwa kuthibitiwa.
- 20.3 Kuthibitisha usajili wa majina ya wachezaji wa mpira wa kikapu.
- 20.4 Kutayarisha kalenda ya TBF.
- 20.5 Kupokea na kujadili taaarifa za kamisheni.
- 20.6 Kupendekeza jina la mlezi
- 20.7 Kujadili na kushughulikia taarifa za utekelezaji wa kazi

- za kila siku za shirikisho ikiwa ni pamoja na taarifa za mapato na matumizi ya kila robo mwaka.
- 20.8 Kupokea, kujadili na kutoa uamuzi juu ya malalamiko na rufaa kadri zitakavyowasilishwa.
 - 20.9 Kuhakikisha kuwa katiba, kanuni na taratibu za mchezo wa mpira wa kikapu zinafuatwa na kuzingatiwa.
 - 20.10 Kutayarisha ajenda za kikao cha Bodi
 - 20.11 Wajumbe wa kamati ya utendaji mmoja mmoja au kwa ujumla wao watawajibika kwenye Bodi ya Utawala na kwenye mkutano mkuu.

IBARA YA 21

KAMISHENI ZA SHIRIKISHO

- 21.1 Kutakuwepo na kamisheni nane za shirikisho.
 - 21.1.1 Kamisheni ya Makocha.
 - 21.1.2 Kamisheni ya Waamuzi
 - 21.1.3 Kamisheni ya watoto wadogo na maendeleo ya mashule
 - 21.1.4 Kamisheni ya Wanawake
 - 21.1.5 Kamisheni ya Mipango na Maendeleo
 - 21.1.6 Kamisheni ya watu wenye ulemavu
 - 21.1.7 Kamisheni ya Tiba ya wanamichezo.
 - 21.1.8 Kamisheni ya ufundi na uendeshaji wa mashindano.
- 21.2 Kila kamisheni itaongozwa na Kamishna ambaye atachaguliwa na mkutano mkuu wa uchaguzi.
- 21.3 Kamishina atakuwa mwenye dhamana ya kuteua na kuongoza kamisheni.
- 21.4 Kamisheni itakutana mara moja kila mwezi ila unaweza kuitishwa mkutano wa dharura wa kamisheni iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.
- 21.5 Kamisheni zitafanya kazi za kila siku kwa siku kwa niaba ya sekretarieti zinazohusiana na kamisheni.

IBARA YA 22

WAJUMBE WA KAMISHENI

- 22.1 Kamishina ataunda kamisheni kwa muundo unaofaa. Mwenyekiti wa vikao vyote vya kamisheni atakuwa ni kamishina mwenyewe.
- 22.2 Kutakuwepo na wajumbe wa kamisheni wasiozidi watano na wasiopungua watatu.
- 22.3 Wajumbe hao watateuliwa na kamishina anayehusika na kuthibitishwa na kamati ya utendaji
- 22.4 Wajumbe watawajibika kwa kamishina mhusika na kwenye kamati ya utendaji.

IBARA YA 23

KAMISHENI YA MAKOCHA

- Kamisheni ya walimu wa mpira wa kikapu itakuwa na majukumu yafuatayo:
 - 23.1 Kuandaa mpango wa maendeleo ya makocha.
 - 23.2 Kusimamia na kuendeleza elimu na viwango vya makocha.
 - 23.3 Kushauri mikoa katika kuweka mipango ya kuendeleza ufundishaji wa makocha na wakufunzi.
 - 23.4 Kuandaa na kusimamia mitaala ya walimu wa mpira wa kikapu pamoja na Wakufunzi katika mikoa na taasisi

- nyingine ili kuhidhinisha vyeti vya madaraja mbalimbali kwa wahitimu.
- 23.5 Kuandaa na kuwasilisha kwenye bodi ya shirikisho sheria na kanuni za waalimu wa mpira wa kikapu.
 - 23.6 Kusimamia na kushirikiana na kamisheni ya Ufundi na Uendeshaji wa mashindano katika kuandaa warsha na mikutano inayojadili na kuchambua matokeo ya kiufundi na kutoa msaada kwa mikoa.
 - 23.7 Kutunza na kuweka takwimu za wachezaji na ushiriki wa timu kwenye mashindano mbalimbali.
 - 23.8 Kuchagua waalimu na wachezaji watakaounda timu ya taifa ya wakubwa.
 - 23.9 Kushirikiana na kamisheni nyingine na vyombo vingine nje ya shirikisho katika kuleta maendeleo ya ufundishaji wa mpira wa kikapu.

IBARA YA 24

KAMISHINA YA WAAMUZI

- 24.1 Kutakuwa na kamisheni ya waamuzi yenye kazi zifuatazo:
- 24.2 Kuandaa na kusimamia mpira wa maendeleo wa waamuzi wote wa mpira wa kikapu katika taifa.
- 24.3 Kuandaa mpango wa mafunzo kwa waamuzi ili kuwawezesha kuwa waamuzi wa kimataifa wanaotambuliwa.
- 24.4 Kuendeleza utaalumu wa waamuzi wa Taifa.
- 24.5 Kutunza na kudhibiti orodha ya waamuzi kila mwaka kwa madaraja tofauti.
- 24.6 Kuwasilisha orodha kwenye kamati ya utendaji ya waamuzi wa Kimataifa na wale wanaotarajiwa kuwa katika orodha hiyo.
- 24.7 Kusimamia Uandaaji wa mafunzo ya waamuzi na makamishina wa michezo kwa kushirikiana na mikoa.
- 24.8 Kushauri shirikisho na kuleta mpango wa kuongeza viwango vya uchezeshaji wa Waamuzi wa Kimataifa.
- 24.9 Kushirikiana na Kamisheni nyingine na Vyombo vingine nje ya Shirikisho katika kuleta maendeleo na uchezeshaji bora wa mpira wa kikapu.

IBARA YA 25

KAMISHENI YA WATOTO WADOGO NA MAENDELEO YA SHULE

- Kamisheni ya watoto wadogo na mashule itakuwa na wajibu na kazi zifuatazo:
- 25.1 Kuandaa mpango wa maendeleo kwa watoto wadogo na vijana kwa kushirikiana na vyama, mashirika ya michezo ya Taifa, Mashule na Vyujo kupanga kalenda rasmi ya mwaka ya mashindano ya mpira wa kikapu.
 - 25.2 Kuandaa na kusimamia sheria maalumu juu ya watoto, pamoja na kuandaa mashindano.
 - 25.3 Kufuatilia na kudhibiti maandalizi ya mashindano ya watoto wadogo na vijana.
 - 25.4 Kuandaa nyaraka za uongozi inayotoa miongozo ya uendeshaji wa mafunzo na mashindano ya watoto chini ya miaka 14 na 17.
 - 25.5 Kushirikiana na vyama husika kuhakikisha kwamba

- mchezo wa mpira wa kikapu unachezwa katika mashule na vyuo nchi nzima.
- 25.6 Kuchagua timu ya Taifa ya Watoto wadogo na vijana kutokana na kiwango chao cha mchezo.
- 25.7 Kushirikiana na kamisheni au vyombo vingine nje ya shirikisho katika kuleta maendeleo ya mpira wa kikapu kwa watoto wadogo na vijana.

IBARA YA 26

KAMISHENI YA WANAWAKE

- Kamisheni ya Wanawake itakuwa na wajibu na kazi zifuatazo:
- 26.1 Kuandaa mpango wa maendeleo ya mpira wa kikapu kwa wanawake.
- 26.2 Kukuza na kuendeleza Mpira wa kikapu kwa wanawake.
- 26.3 Kuwahamasisha wanawake kushiriki mashindano kama wachezaji, walimu, waamuzi, mameneja na makamisaa wa michezo.
- 26.4 Kufuatilia na kudhibiti maandalizi ya mashindano ya Mpira wa kikapu ya Wanawake kwa kusaidiana na Kamisheni ya Ufundi na uendeshaji wa mashindano.
- 26.5 Kutoa ripoti kwa Kamati ya Utendaji na Bodi ya Shirikisho juu ya maendeleo ya mipango ya kiufundi, Program za TBF za Wanawake na kubuni mashindano mbalimbali.
- 26.6 Kuandaa nyaraka na miongozo inayotoa habari juu ya matokeo ya mashindano mbalimbali.
- 26.7 Kutayarisha majarida, vipeperushi na vifaa vya kufundishia kama vile Video, Kanda, Filamu kwa ajili ya Walimu, waamuzi na wataalamu wengine.
- 26.8 Kuarifu vyama vya mikoa juu ya viandikia na vifaa vingine vinavyohitajika kwa ajili ya mafunzo na mazoezi ya timu kwa ngazi zote.
- 26.9 Kuandaa programu ya mafunzo ya Taifa kwa wanawake –walimu, Makamisaa na wamuzi, aidha kuandaa vitini mbalimbali vya kufundishia.
- 26.10 Kushirikiana na kamisheni nyingine au vyombo vingine nje ya shirikisho katika kuleta maendeleo ya Mpira wa kikapu nchini.

IBARA YA 27

KAMISHENI YA MIPANGO NA MAENDELEO

- Kamisheni ya mipango na maendeleo itakuwa na wajibu na kazi zifuatazo:
- 27.1 Kuratibu mipango na maendeleo ya kila kamisheni
- 27.2 Kutambua maeneo yanayohitaji utaalumu katika utawala na uongozi.
- 27.3 Kupata wataalamu na washauri katika maeneo yanayohusika.
- 27.4 Kujenga sura nzuri ya mchezo wa mpira wa kikapu nchini.
- 27.5 Kuongeza ukubwa wa soko na thamani ya mpira wa kikapu miongoni mwa michezo mingine
- 27.6 Kushirikisha jumuiya zisizo za mchezo wa mpira wa kikapu katika kukuza mchezo huo.

- 27.7 Kupendekeza mipango ya ushindi wa timu za taifa kwa ajili ya mashindano ya kimataifa.
- 27.8 Kufafanua bidhaa za mpira wa kikapu zitakazouzika katika soko.
- 27.9 Kupanga na kutekeleza miradi itakayoweza kusaidia kuendesha makadilio ya shirikisho.
- 27.10 Kuongeza kiwango cha ufadhili maeneo yote na shughuli zote za TBF.
- 27.11 Kuhakikisha kuwa shirikisho linajitegemea.
- 27.12 Kuhakikisha kuwa ufadhili unaendana na mchezo wa mpira wa kikapu.
- 27.13 Kuhakikisha kuwa mashindano yote yanafanyika katika hali kwamba wafadhili wanapata wanachotaka na kikapu.
- 27.14 Kushirikiana na kamisheni nyingine katika kuleta maendeleo ya mpira wa kikapu
- 27.15 Kuweka mipango ya kulipatia shirikisho mapato na udhibiti wake.

IBARA YA 28

KAMISHENI YA WALEMAVU

Kamisheni ya walemavu ya mpira wa kikapu itakuwa na majukumu yafuatayo:

- 28.1 Kuandaa mpango kwa walemavu ili waweze kushiriki uchezaji wa mpira wa kikapu wa namna tofauti.
- 28.2 Kuamsha hamasa miongoni mwa walemavu ili washiriki mchezo wakiwa wachezaji, waamuzi, viongozi na washabiki wa mpira wa kikapu.
- 28.3 Kuandaa na kusimamia sheria maalumu za mpira wa kikapu wa wenyeviti wa mpira wa kikapu unaochezwa na walemavu wakiwa wamekaa chini.
- 28.4 Kuandaa miongozo na kusimamia mafunzo ya mpira wa kikapu kwa walemavu.
- 28.5 Kutayarisha majarida, vipeperushi na vifaa vya kufundishia kama vile video, kanda, filamu kwa ajili ya waalimu, waamuzi na wataalamu.
- 28.6 Kusimamia mashindano yanayohusu mpira wa kikapu kwa walemavu.
- 28.7 Kushirikiana na kamisheni nyingine na vyombo vingine nje ya shirikisho katika kuleta maendeleo ya mpira wa kikapu kwa walemavu.

IBARA YA 29

KAMISHENI YA TIBA YA WANAMICHEZO

Kamisheni ya Tiba ya Wanamichezo itakuwa na majukumu yafuatayo:

- 29.1 Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango na maendeleo ya Tiba kwa wanamichezo utakaosaidia kukuza viwango vya uchezaji pamoja na kucheza mpira wa kikapu kwa muda mrefu.
- 29.2 Kuthibiti utumiaji wa madawa ya kuongeza nguvu kwa wachezaji
- 29.3 Kuthibiti na kusimamia sheria zinazokataza waalimu, waamuzi, makamisaa na wachezaji kutokujihusisha na

- 29.4 mchezo wakati wakiwa wamelewa. Kutayarisha majarida, vipeperushi na vifaa vingine vya kufundishia afya ya wanamichezo.
- 29.5 Kusimamia na kudhihinisha watoa huduma ya kwanza kwenye mashindano yoyote yanayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania.
- 29.6 Kutoa mafunzo kwa wachua misuli na Wasimamizi wa afya za wachezaji kwenye vilabu kwa kushirikiana na mikoa.
- 29.7 Kuelekeza na kusimamia lishe bora ya wanamichezo wakati wa mazoezi na mashindano.
- 29.8 Kushirikiana na kamisheni nyingine na vyombo vingine nje ya shirikisho katika kuleta maendeleo ya mpira wa kikapu kwa kuwa na wanamichezo wenye afya bora.

IBARA YA 30

KAMISHENI YA UFUNDI NA UENDESHAJI WA MASHINDANO

Kamisheni ya ufundi na uendeshaji itakuwa na kazi zifuatazo:

- 30.1 Kuandaa mpango wa maendeleo ya kiufundi wa Shirikisho.
- 30.2 Kuandaa sheria na kanuni za mashindano ya Shirikisho.
- 30.3 Kufuatilia na kuthibiisha maandalizi ya mashindano ya TBF Kwa msaada wa Sekretarieti.
- 30.4 Kutoa ripoti kwa kamati ya utendaji wa Bodi ya Shirikisho, maendeleo ya mipango ya kiufundi, programu za TBF.
- 30.5 Kuandaa nyaraka za miongozo inayotoa habari juu ya matokeo ya mashindano mbalimbali.
- 30.6 Kutayarisha majarida, vipeperushi na vifaa vya kufundishia kama vile video, kanda filamu kwa ajili walimu, waamuzi na wataalamu wengine.
- 30.7 Kubuni miradi yenye mwelekeo wa kielimu na mafunzo.
- 30.8 Kuandaa na kusimamia ratiba za mashindano mbalimbali.
- 30.9 Kushirikiana na kamisheni nyingine na vyombo vingine nje ya shirikisho kuleta maendeleo ya mpira wa kikapu.

SURA YA IV UCHAGUZI

IBARA YA 31

MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI

- 31.1 Kutakuwepo na mkutano mkuu wa uchaguzi kila baada ya miaka mine.
- 31.2 Mkutano mkuu unaweza kuridhia na kuongeza muda wa kuendelea na uongozi uliopo au unaweza kuteua kamati ya muda ya uongozi na kuipa kipindi maalumu cha kuongoza na kuitisha mkutano wa uchaguzi.
- 31.3 Siku 30 zikipita baada ya kipindi cha uongozi kumalizika bila ridhaa ya mkutano mkuu, viongozi wanaomaliza muda wao watahesabika kuwa wamejivua uongozi.
- 31.4 Katika hatua hii hapo juu (30.4) B.M.T. litaandaa utaratibu wa kuitisha uchaguzi ili kuchangua kipindi cha uongozi kumalizika.

- 31.5 Mkutano mkuu ukitoa ridhaa yake, kwa uongozi uliopo madarakani kama unavyoelezeka kataika (aya 30.3 hapo juu) ridhaa hiyo itakuwa kwa kipindi kisichozidi siku 90 (tisini tu) baada ya siku ya mwisho ya kipindi cha uongozi kumalizika.
- 31.6 Fomu za wagombea wa T.B.T zitatolewa na B.M.T. Aidha BMT itafanya uchambuzi wa majina ya wagombea kwa kuzingatia sifa za wagombea kama zilivyoainishwa katika katiba ya T.B.F.
- 31.7 Shughuli za uchambuzi zitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za T.B.F na zile za FIBA.
- 31.8 Uchaguzi wa T.B.F utakuwa wa haki na wazi na utasimamiwa na BMT.
- 31.9 Mkutano mkuu wa uchaguzi utachagua na kujaza nafasi zifuatazo:
 - 31.9.1 Rais wa Shirikisho
 - 31.9.2 Makamu wa Rais
 - 31.9.3 Katibu Mkuu
 - 31.9.4 Katibu Mkuu msaidizi
 - 31.9.5 Mweka Hazina
 - 31.9.6 Kamishina wa mipango na maendeleo
 - 31.9.7 Kamishina wa makocha
 - 31.9.8 Kamishina wa ufundi na uendeshaji mashindano
 - 31.9.9 Kamishina wa waamuzi
 - 31.9.10 Kamishina wa wtoto wadogo na maendeleo ya shule
 - 31.9.11 Kamishina wa wanawake
 - 31.9.12 Kamishina wa watu wenye ulemavu
 - 31.9.13 Kamishina wa tiba ya wanamichezo.

IBARA YA 32

WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI

- 32.1 Wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi ni wale tu ambao vyama vyao vitakuwa vimesajiliwa na havidaiwi ada ya mwaka.
- 32.2 Mwenyekiti na katibu kutoka kila mkoa mwanachama watakuwa wajumbe wenye haki ya kupiga kura.
- 32.3 Mwenyekiti na makatibu kutoka vyama vishiriki watakuwa wajumbe wenye haki ya kura moja.
- 32.4 Mchezaji mwakilishi kutoka kila mkoa mwanachama ambaye atakuwa na haki ya kupiga kura.
- 32.5 Wajumbe wa kamati ya utendaji wanaomaliza muda waliotajwa katika ibara ya 31.9 ambao hawatapiga kura wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi.
- 32.6 Msimamizi wa uchaguzi mkuu kutoka BMT ambaye hatapiga kura.

IBARA YA 33

SIFA ZA WAGOMBEA UONGOZI

- Wagombea wa uongozi wa Shirikisho wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:
 - 33.1 Awe na umri usiopungua miaka 25, isipokuwa wale wanaogombea nafasi ya Rais na Makamu wa Rais ambao wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka 30.
 - 33.2 Awe raia wa Tanzania.
 - 33.3 Awe na elimu angalau ya kidato cha Nne.
 - 33.4 Awe na ufahamu juu ya Shirikisho na Taasisi zake,

- ajue shughuli zake na uendeshaji.
- 33.5 Awe na uzoefu wa kitaifa na wa kimataifa juu ya nafasi ya uongozi anayogombea.
- 33.6 Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya kiswhilil na kiingereza ambazo zinatumiwa na Shirikisho.
- 33.7 Awe na moyo wa kujitolea na awe na nafasi ya kutoa muda wake kwa kutumikia Shirikisho bila ya malipo kwa kipindi tofauti angalau siku 30 kwa mwaka. Akishiriki katika vikao, warsha na mashindano.
- 33.8 Awe hajapatikana na hatia ya kosa lolote la jinai hususa linalogusa na kushusha hadhi, utu na haiba mbele ya jamii (kama wizi , mauaji, kubaka, madawa ya kulevya n.k.)
- 33.9 Awe na akili timamu na hajawahi kuugua ugonjwa wa akili.
- 33.10 Wagombea wa nafasi ya Rais na Makamu wake , lazima wawe na elimu na uzoefu w kutosha wa mambo ya utawala wa michezo, hasa wawe wameisha wahi kuongoza mchezo wa mpira wa kikapu kwa ngazi yoyote nchini.
- 33.11 Awe amewahi kuwa mchezaji wa mpira wa kikapu, au kuhudhuria mafunzo ya ualimu wa mpira wa kikapu, uamuzi, utawala wa michezo, tiba ya wanamichezo, au utunzaji na utengenezaji wa viwanja vya michezo.

IBARA YA 34

KIPINDI CHA UONGOZI

- 34.1 Kipindi cha uongozi wa shirikisho ni miaka mine.
- 34.2 Kiongozi yoyote wa TBF anaweza kuchaguliwa kuongoza kwa vipindi viwili mfululizo.
- 34.3 Rais wa Shriikisho, Makamu na Katibu Mkuu iwapo wameongoza kwa vipindi viwili mfululizo hawataruhusiwa kugombea nafasi aliyo nayo, isipokuwa anaweza kugombea nafasi yoyote katika shirikisho.
- 34.4 Kiongozi ambae atajiuzulu uongozi katika nafasi Fulani baada ya kuitumikia kwa zaidi ya miaka mitatu atahesabika kuwa ametumikia kipindi kizima.
- 34.5 Endapo kutatokea nafasi ya wazi ya uongozi kutokana na sababu yoyote, nafasi hiyo itajazwa na mamlaka zenye dhamana hiyo kwa mujibu wa katiba hii katika kikao kinachofuata.

SURA YA V

VIONGOZI WA SHIRIKISHO KAZI NA MADARAKA

IBARA YA 35

VIONGOZI WA SHIRIKISHO

Kutakuwa na viongozi wa shirikisho wafuatao:
 Rais wa Shirikisho
 Makamu wa Rais
 Katibu Mkuu
 Katibu Mkuu msaidizi
 Mweka Hazina
 Kamishina wa mipango na maendeleo
 Kamishina wa wtoto wadogo na maendeleo ya shule

Kamishina wa wanawake
Kamishina wa watu wenye ulemavu
Kamishina wa makocha
Kamishina wa waamuzi
Kamishina wa tiba ya wanamichezo.
Kamishina wa ufundi na uendeshaji mashindano

IBARA YA 36

KAZI, MADARAKA, NA WAJIBU

- 36.1.0 Rais wa Shirikisho
- 36.1.1 Atakuwa kiongozi mkuu wa shirikish mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa madhumuni ya shirikisho.
- 36.1.2 Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, na vikao vya bodi vya shirikisho.
- 36.1.3 Atapitisha malipo kwa kutia saini kwenye hundi za shirikisho.
- 36.1.4 Ataweka saini mikataba yote inayohusu Shirikisho.
- 36.1.5 Atahakikisha kuwa shughuli zote za kila siku za Shirikisho zinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za ufanisi.
- 36.1.6 Atafuatilia kuona kuwa maagizo yote yatokay kwenye vyombo vya juu kwa Shirikisho yanatekelezwa ipasavyo
- 36.1.7 Atakuwa na kura ya ziada ya uamuzi endapo kunatokea sare ya kura, isipokuwa kwa suala la uchaguzi.
- 36.1.8 Atawajibika kulinda na kuitetea kwa nguvu zake zote katiba ya Shirikisho.
- 36.1.9 Atawajibika kwenye bodi ya shirikisho.
- 36.1.10 Atakuwa msemaji mkuu w shirikisho
- 36.1.11 Atakuwa msimamizi na Mdhibiti Mkuu wa shughuli na maendeleo ya watumishi wote walioajiriwa na Shirikisho.
- 36.1.12 Anaweza kufanya maamuzi yoyote kwa faida ya shirikisho na kuyatolea maelezo baadaye kwenye vikao vya shirikisho.
- 36.1.13 Anaweza kushiriki katika kikao chochote cha shirikisho kwenye ngazi ya chini.

- 36.2.0 Makamu wa Rais
- 36.2.1 Atakuwa na kazi na madaraka yote ya Rais kama yalivyoainishwa katika aya ya 1 ya ibara hii, iwapo Rais wa Shirikisho hayupo.
- 36.2.2 Atajishughulisha na ustawi wa matawi ya shirikisho na kuhamasisha kujiunga kwa wanachama wapya.
- 36.2.3 Atamwakilisha Rais na kufanya kazi atakazoelekezwa naye
- 36.2.4 Atawajibika kwenye bodi ya shirikisho.

- 36.3.0 Katibu Mkuu
- 36.3.1 Atakuwa afisa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa madhumuni ya shirikisho.
- 36.3.2 Atakuwa mhamasishaji mkuu wa shughuli za shirikisho na mwenezi wa mpira w kikapu.

- 36.3.3 Atakuwa ndie afisa mhasibu mkuu wa shirikisho
- 36.3.4 Atakuwa katibu wa mkutano mkuu Bodi ya shirikisho kamati ya Utendaji.
- 36.3.5 Atapitisha malipo kwa kutia saini hundi za shirikisho na kuidhinisha malipo ya shirikisho kwa mujibu wa kanuni za fedha za shirikisho.
- 36.3.6 Atasimamia utayarishaji wa makisio ya mapato/matumizi ya mwaka pamoja na taarifa ya fedha ya chama ya robo mwaka.
- 36.3.7 Atakuwa msimamizi na mdhibiti mkuu wa shughuli za maendeleo ya watumishi walioajiriwa na TBF.
- 36.3.8 Anaweza kushiriki katika kikao cha kamisheni yoyote au kamati nyingine yeyote itakayoundwa.
- 36.3.9 Atakuwa mwenyekiti wa kamati ya utendaji.

- 36.4.0 Katibu Mkuu Msaidizi
- 36.4.1 Atafanya kazi zote za katibu mkuu iwapo hayupo.
- 36.4.2 Atakuwa mwenyekiti wa vikao vya kuendesha mashindano mbalimbali ya chama.
- 36.4.3 Atakuwa ni afisa utawala na utumishi wa shirikisho.
- 36.4.4 Atawajibika kwa Katibu Mkuu na kamati ya Utendaji.
- 36.4.5 Atafanya kazi nyingine atakazoagizwe n kupangiwa na Katibu Mkuu au Sekretarieti.
- 36.4.6 Atakuwa katibu mkuu wa kamati ya utendaji.
- 36.4.7 Atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti, ikitokea kwamba Katibu Mkuu ambae ni mwenyekiti wa kamati hii hawezi kufika kwenye kikao hicho.
- 36.4.8 Ikitokea hali iliyotajwa katika aya ya 36.4.7 wajumbe waliotimia wa sekretarieti watamchagua miongoni mwao kuwa katibu wa muda wa kikao hicho.

- 36.5.0 Mweka Hazina
- 36.5.1 Atakuwa Mshauri Mkuu wa TBF kwa masuala yahasuyo fedha na usimamizi wake.
- 36.5.2 Atatunza fedha na vitabu vya hesabu na nayaraka zote zihusuzo fedha.
- 36.5.3 Atakuwa mmojawapo wa kutia saini hundi za Shirikisho
- 36.5.4 Ataandaa makisio ya mapata ya shirikisho na matumizi ya fedha kwa mwaka na kuwasilisha kwenye kamati ya Utendaji.
- 36.5.5 Atatayarisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za shirikisho kwa mwezi, miezi mitatu nay a mwaka na kuwasilisha kwa katibu ili ijadiliwe na kamati tayariri kwa ukaguzi wa mahesabu
- 36.5.6 Atabuni njia mbalimbali za kuongeza mapato ya chama
- 36.5.7 Atawajibika kwa katibu mkuu na kwenye kamisheni ya mipango na maendeleo.

- 36.6.0 Makamishina wa Shirikisho
- 36.6.1 Watakuwa Wenyeviti wa vikao vyote vinavyohusu kamisheni zao.
- 36.6.2 Watakuwa viongozi wenye dhamana ya kusimamia na

- kutekeleza shughuli zote zilizo chini ya kamishenini zao.
- 36.6.3 Watahusika na utawala wa siku kwa siku wa Kamisheni wanazoziongoza
 - 36.6.4 Watateua wajumbe wa kamisheni wanazoongoza.
 - 36.6.5 Watawajiba mmoja mmoja au jumla kwenye kamati ya utendaji.
 - 36.6.6 Watawakilisha shirikisho kwenye kongamano zinazohusiana na kamisheni zao.
 - 36.7.0 Wajumbe wa kamati za TBF
 - 36.7.1 Watasimamia vituo vya mashindano
 - 36.7.2 Watakuwa watekelezaji wa maamuzi ya kamisheni zao
 - 36.7.3 Watakuwa ni nguzo muhimu za shirikisho katika utendaji wa siku kwa siku.
 - 36.7.4 Watawakilisha makamishina kwenye makongamano na warsha mbalimbali ndani na nje ya nchi.
 - 36.7.5 Watawajibika kwenye kamisheni zao na kwa kamishina mhusika.
 - 36.7.6 Watachagua katibu wa Kamisheni kutoa miongoni mwao.

IBARA YA 37

MLEZI NA BARAZA LA WADHAMINI

- 37.1.0 Kutakuwepo na Mlezi atakayeteuliwa na Bodi kuthibitishwa katika mkutano mkuu.
- 37.1.2 Mlezi atakuwa mshauri mkuu wa mambo yote ya maendeleo ya mpira wa kikapu na pia atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini.
- 37.1.3 Mlezi atashika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mine lakini anaweza kuchaguliwa tena.
- 37.1.4 Mlezi atakuwa Mshauri wa Shirikisho na atalinda na kuitetea katiba ya shirikisho.
- 37.1.5 Mlezi anaweza kuhudhuria kikao chochote cha shirikisho katika ngazi yoyote.
- 37.2.0 Baraza la Wadhamini
- 37.2.1 Kutakuwepo na baraza la wadhamini litakaloteuliwa na bodi na kuthibitishwa na mkutano mkuu.
- 37.2.2 Baraza la wadhamini litaundwa na wajumbe wane, akiwemo mlezi wa Raisi wa Shirikisho ambaye ni “ex officio”.
- 37.2.3 Wajumbe wa Baraza la Wadhamini watateuliwa na Bodi na kuthibitishwa na mkutano mkuu.
- 37.2.4 Wajumbe wa baraza la Wadhamini watashikiria nafasi hizo kwa kipindi cha miaka minne lakini wanaweza kuteuliwa tena.
- 37.2.5 Mali yote ya shirikisho inayoondosheka na isisyoondosheka itakuwa chini ya miliki ya baraza la wadhamini.

SURA YA VI MIGOGORO NA RUFAA

IBARA YA 38 MIGOGORO

- 38.1 Hairusiwa kwa mtu, chombo, klabu au shirikisho kufikisha suala la mgogoro wowote dhidi ya TBF katika mahakama, isipokuwa kwa masuala ya ubadhilifu au wizi wa fedha au mali za Shirikisho.
- 38.2 Migogoro yoyote itatatuliwa kwa kufuata masharti na taratibu zilizomo katika katiba hii na kufuata sheria na kanuni za BMT.
- 38.3 Mtu, klabu, mkoa au chombo chochote kinacho jishirikisha na TBF kitakacho kiuka masharti ya aya ya kwanza ya ibara hii, kitachukuliwa mojawapo ya hatua zifuatazo.
 - 38.3.1 Kusimamishwa uanachama
 - 38.3.2 Kusimamishwa au kusitisha ushiriki wake katika mashindano husika au.
 - 38.3.3 Kupigwa marufuku kuandaa na kuendesha mchezo wa mpira wa kikapu.
- 38.4 Mtu au chombo chochote, ikiwa ni pamoja na mchezaji, mwamuzi, mwalimu, kiongozi yeyote wa mpira wa kikapu ndani ya nchi, anayo haki ya kukata rufaa kwa chombo cha ngazi ya juu kuliko kile kilichotoa uamuzi, kupinga maamuzi yaliyotolewa dhidi yake.
- 38.5 Rufaa zote za mpira wa kikapu, zitafuluata utaratibu kama ilivyo ainishwa kwenye kanuni za Shirikisho.

SURA YA VII FEDHA ZA SHIRIKISHO

IBARA YA 39 MAPATO:

- 39.1 Fedha zote zitakazopatikana kutokana na shughuli za mpira wa kikapu kwenye kamisheni au kamati yoyote ndogo ya TBF, zitakuwa ni mali ya shirikisho na zitatumika kwa kusudio lake lililofanywa kukusanywa kwake.
- 39.2 Bodi inaweza kutoa idhini ya kuhamisha akaunti au fedha za shirikisho na kuziweka kwenye udhibiti wa taasisi nyingine, mkoa kamisheni au kamati ndogo.
- 39.3 Mapato ya TBF yatatokana na:-
 - 39.3.1 Viingilio kutokana na wanachama wapya
 - 39.3.2 Ada za wanachama kila mwaka.
 - 39.3.4 Ada inayo lipwa na waandaji wa mashindano ambao si wanachama.
 - 39.3.5 Ada ya leseni za waamuzi wa kitaifa
 - 39.3.6 Viingilio katika mashindano kutoka kwenye timu na viingilio vya uwanjani
 - 39.3.7 Ruzuku kutoka serikalini, BMT, TOC au mashirikisho ya kimataifa ya mpira wa kikapu
 - 39.3.8 Mapato yatokanayo na kutolewa kwa leseni ya kutumia haki ya shirikisho kwenye matangazo ya biashara.
 - 39.3.9 Udhamini mbalimbali

- 39.3.10 Faini zitokanazo na adhabu kwa makosa mbalimbali.
39.3.11 Michango ya hiari.
39.1.12 Shughuli zitakazoendeshwa na TBF kuchangia shughuli maalumu za mpira wa kikapu.
- 39.4 Wakala wa matangazo anaweza kutumika kutafuta udhamini wa matangazo au kuwakilisha shirikisho kwenye majadiliano yahasuyo kifungu 39.3.8 na kulipwa asilimia ya mapato kadri ya mapatano.
- 39.5 Wakala au washauri watakaoweza mkataba wa udhamini wa shughuli za shirikisho, watalipwa asilimia itakayo kubalika, ambayo itakuwa imeongezwa kwenye mkataba wakati wa majadiliano.
- 39.6 Haki za udhamini na vipengele vya mikataba vitalindwa na kuheshimiwa.

IBARA YA 40 MATUMIZI

- 40.1 Fedha za shirikisho zitatunzwa na Benki katika Akaunti ya TBF.
- 40.2 Malipo yote yatafanywa kufuata kanuni za fedha na kumbukumbu zote kutunzwa katika vitabu vya hesabu shirikisho.
- 40.3 Fedha zitatolewa kutoka Benki baada ya kuandikwa kwa hundi ambayo itatiwa sahihi na maafisa wawili kati ya wafuatao kama kanuni zitakavyoeleza:-
- Rais wa Shirikisho
 - Makamu wa Rais
 - Katibu Mkuu
 - Mweka hazina
 - Kamishina
- 40.4 Malipo yoyote ya fedha inayozidi Shs. 250,000/= ni lazima yaidhinishwa na Rais wa shirikisho.

IBARA YA 41 HESABU

- 41.1 Mwaka wa fedha wa shirikisho utakuwa Januari hadi Desemba kila mwaka.
- 41.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Wakaguzi wa Hesabu wa nje zitawasilishwa kwenye mkutano wa bodi ya Shirikisho kila mwaka.
- 41.3 Wakaguzi wa Hesabu watateuliwa na mkutano mkuu wa TBF.
- 41.4 Rais wa Shirikisho, Makamu wa Rais, katibu mkuu na kamishina wa mipango na maendeleo wanaweza kuitisha na kuangalia utunzaji wa vitabu vya hesabu kutoka kwa mtunza hazina wakati wowote ikibidi.
- 41.5 Nakala ya Taarifa ya hesabu itapelekwa kwa Mwenyekiti Bodi ya wadhamini.
- 41.6 Mali za Shirikisho lazima zinakiliwe katika daftari la mali za TBF na kutunzwa kwa mujibu wa sheria.

SURA YA VIII
HATI MILIKI, NEMBO, BENDER NA LUGHA

IBARA YA 42
BENDERA

- 42.1 Shirikisho litakuwa na Bendera yake yenye rangi ya maji ya Bahari na nembo ya shirikisho katikati.
- 42.2 Bendera itapeperushwa na wajumbe wa bodi na kwenye ofisi za Shirikisho.
- 42.3 Bendera itapeperushwa kwenye mashindano yote yanayotambuliwa rasmi na shirikisho.

IBARA YA 43
NEMBO

- 43.1 Kutakuwepo na nembo ya shirikisho.
- 43.2 Nembo ya Shirikisho ina alama ya Goli la mpira wa kikapu, ramani ya Tanzania iliyonakishiwa kwa rangi za Bendera ya Tanzania inayoingia ndani ya kikapu.
- 43.3 Ndani ya ramani ya Tanzania, kutakuwepo na mpira wa kikapu na kifupisho cha shirikisho.
- 43.4 Mpira na Ramani ya Tanzania, kutakuwepo na mpira wa kikapu na kifupisho cha shirikisho.
- 43.5 Ramani inayoingia kwenye goli la mchezo ni ishara ya azma ya kufanya Tanzania kuwa nchi ya mchezo wa mpira wa kikapu.

IBARA YA 44
LUGHA

- 44.1 Lugha rasmi katika shughuli zote za Shirikisho ni Kiswahili na kiingereza. Lugha hizi pekee ndizo zitakazo tumika katika vikao na mawasiliano mengine.
- 44.2 Ikitokea kutokueleweka au kuchanganyika kwa baadhi ya vifungu vya katiba hii: Tafsiri ya lugha ya Kiswahili itafuatwa.

IBARA YA 45
UAMUZI WA KUVUNJA SHIRIKISHO

- 45.1 Shirikisho linaweza kuvunjwa kwa uamuzi wa mkutano mkuu ambao Wadhamini na mlezi wataalikwa na kutoa ushauri wao, kabla ya kupigwa kura za siri na uamuzi huo.
- 45.2 Uamuzi wa kuvunja TBF utafikiwa kwa kura za siri kwa wajumbe zaidi ya robo tatu (3/4) kukubali uamuzi huo.

IBARA YA 46
KUPITISHA KATIBA

- 46.1 Katiba hii itaanza kutumika kuanzia.....
- 46.2 Kwa tamko la pamoja la mkutano mkuu maalumu wa katiba uliofanyika tarehe 21 Octoba 2001, katika ukumbi wa mkuu wa mkoa wa Dodoma unafuta katiba ya sasa ya Chama cha Mpira wa kikapu Tanzania. (BATA).

MWISHO